



UNIVERSITÄT
BAYREUTH

WARSHA - KISWAHILI

KAULI MBIU

*TAFSIRI NA UKALIMANI: NAFASI
NA CHANGAMOTO ZAKE*

Disemba 2-3, 2021

Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret

**Ratiba na
Kitabu cha Ikisiri**



Prof Isaac Kosgey
Makamu Mkuu, Chuo Kikuu cha Moi



Prof. Dkt. Peter Simatei
Mkurugenzi,
African Cluster Centre Moi University



Prof. T. Michael Mboya
Mratibu wa TAALUMA,
African Cluster Centre Moi University.



Prof. Mary Wahome

Mtiva,

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii



Prof Mosol Kandagor

Mtiva Mshiriki, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii

Moi University African Cluster Centre - Profile

This workshop is just one of the many planned research activities of the Moi African Cluster Centre of Excellence in African studies for the year 2021. The Moi University African Cluster Centre (Moi-ACC) is housed in the School of Arts and Social Sciences (SASS) of Moi University. The overriding objectives of the Moi University School of Arts and Social Sciences are to offer interdisciplinary teaching and research in the broad field of African studies and to act as the center where all other Africa-focused scholarship in Moi University coalesce. Within the context of these objectives, and building on the very strong tradition of exploring and interrogating diverse ways of knowing Africa that has developed in the School in the three and a half decades of its existence, the Moi-ACC is envisioned as a hub of outstanding inter-, multi- and transdisciplinary research and conversations that contribute to the greater understanding of Africa in ways that enable the addressing of significant issues affecting the continent. At Moi-ACC research is carried out under the following sections: Affiliations, Arts and Aesthetics, Mobilities, Moralities, Knowledges and Learning. The research projects that are currently on-going in these sections are: Regional integration in Eastern and Southern Africa: An appraisal of the frameworks for interactive markets, effective governance and human rights protection; East African Asian Writing and the Emergence of a Diasporic Subjectivity; Framing Identities from Human Agency Mobility on the Kenya-Uganda Highway; Changing Life Projects: African Identities, Moralities and Wellbeing; Pots, Fire and Gourds: A (Re)presentation of African Knowledge Systems; and Mediated and Mediatization of Islamic Knowledge in Kenya: Educational Institutions, Media Technologies and Performative Aesthetics.

Prof. Dr. Peter Simatei
Director,
Moi African Cluster Centre.

Mawasiliano kutoka kwa Mratibu wa Warsha

Ulimwengu wa sasa unadhihirisha uchangamani wa hali ya juu wa watu, tamaduni, taaluma, asasi na taasisi, kwa kutaja tu baadhi. Katika ulimwengu unaokwenda kwa kasi, nyenzo mbalimbali za mawasiliano zinatumika. Nyenzo hizo huwaunganisha pamoja wanajamii wenyewe wingilugha na wingiutamaduni. Utangamano huo unafanikishwa pakubwa na kuwepo kwa taaluma pacha za tafsiri na ukalimani. Taaluma hizi huchukua nafasi kubwa katika kudumisha na “kukusanya mawe ya Babeli yaliyotapakaa kote ulimwenguni” na kuyaweka pamoja kwa ushikamani mwafaka. Aidha, tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo zimechangia kuunda ulimwengu kuwa kijiji na kuimarisha utangamano wa watu pamoja na usambazaji wa maarifa. Hata hivyo, licha ya mchango mkubwa katika jamii, taaluma hizi pacha na zenyе historia ndefu, yaani tafsiri na ukalimani hazijatambuliwa na kupewa nafasi yake inavyostahili katika jamii, hususan katika Bara la Afrika. Pia, zinakabiliwa na changamoto za kinadharia, kiutendaji na kimitazamo. Warsha hii itaangazia masuala haya na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike ili kukabiliana na hali hii.

**Prof. Mosol Kandagor
Mratibu**



RATIBA YA WARSHA

SIKU YA KWANZA ALHAMISI 02/12/2021		
Saa/Muda	Shughuli	Mhusika/Wahusika
3:00 – 4:00	Usajili	Caroline, Enos, Lilian, Prisca, Wilberforce
Sehemu ya Kwanza: Ufunguzi Mwenyekiti: Dkt. Mohamed Mohamed Katibu: Dkt. Allan Opijah		
4:00 – 4:15	Utangulizi wa Warsha	Prof. Mosol Kandagor Mtiva Mshiriki, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za jamii na Mrabu wa Warsha
4:15 – 4:25	Hotuba Fupi	Prof. Tom Mboya Mratibu wa Taaluma Moi-ACC
4:25 – 4:35	Hotuba Fupi	Prof. Mary Wahome Mtiva, Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii
4:35-4:45	Hotuba Fupi	Prof. Peter Simatei Mkurugenzi, Moi-ACC
4.45– 5:00	Ufunguzi Rasmi	Prof. Isaac S. Kosgey Makamu Mkuu wa Chuo Chuo Kikuu cha Moi
5:00 – 5:15	Chai	Wote
Sehemu ya Pili: Makala Elekezi 1 Mwenyekiti: Prof. S. Obuchi Katibu: Dkt. A. Opijah		
5:15-6:00	Makala Elekezi 1: Tafsiri na Ukalimani: Nafasi na Changamoto zake	Prof. P. Iribemwangi Chuo Kikuu cha Nairobi
Sehemu ya Tatu: Mawasilisho ya Makala Mwenyekiti: Dkt. Mbwarali Kame Katibu: Mahero Toboso		
6:00 – 6:20	Ufasiri katika Sekta ya Sheria Nchini Uganda: Changamoto na Mustakabali	Dkt. Caroline Asiimwe Chuo Kikuu cha Makerere
6:20 – 6:40	Tafsiri, Utahozi na Uakronimu katika Ukuzaaji wa Istilahi za Utafiti wa Kiswahili katika Kiwango cha Uzamilifu	Dkt. Susan Choge Chuo Kikuu Kishirikishi cha Kotalel Samoei
6.40-7.00	TAFSIRI NA NAFASI YAKE KATIKA MAENDELEO YA FASIHI YA KISWAHILI	Dkt. Mwanakombo Mohamed Chuo Kikuu cha Moi

7:00 – 7:30	Maswali, Maoni na Majibu	
7:30 – 8:30	Chamcha	
Sehemu ya Nne: Makala Elekezi 2 Mwenyekiti: Dkt. Caroline Asiimwe Katibu: Dkt. Mahero Toboso		
8:30 – 9:10	NAFASI YA TAFSIRI NA UKALIMANI KATIKA UMAJUMUI WA KIAFRika: MAFANIKIO, CHANGAMOTO, SULUHISHO	Dkt. Hadija Jilala Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Sehemu ya Tano: Mawasilisho ya Makala Mwenyekiti: Dkt. Magdaline Wafula Katibu: Dkt. Sophia Serem		
9:10 – 9:40	Tafsiri ya Kiswahili katika Mwongo wa Lugha Asili (2022 - 2032)	Prof. Inyani Simala
9:40 – 10:00	Uwezekano ya Kiswahili kutumika kama Lugha ya Sheria Nchini Kenya	Dkt. Chacha Mwita Chuo Kikuu cha Kenyatta
10.00-10:20	CHANGAMOTO ZA TAFSIRI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI: MFANO WA <u>NITAOLEWA NIKIPENDA</u> (NGUGI WA THIONG’O)	Dkt. Joseph. Gakuo
10:20-10:50	Maswali, Maoni na Majibu	
10:20 – 10:40	Chai	
SIKU YA PILI IJUMAA 03/12/2021		
Sehemu ya Sita: Makala Elekezi 3 Prof. P. Iribemwangi Katibu: Dkt. Mwanakombo Mohamed		
03:00 – 3:40	DHIMA YA TAFSIRI NA UKALIMANI KATIKA MAENDELEO: MTAZAMO WA KIDAYAKRONIA	Prof. Miriam Mwita Chuo Kikuu cha Baraton
Sehemu ya Saba: Mawasilisho ya Makala Mwenyekiti: Dkt. A. Sawe Katibu: Dkt. Mbwarali Kame		
3:40 – 4:00	Tafsiri kama Daraja la Utoshelevu wa Chakula Barani Afrika	Gitonga Josephat Chuo Kikuu cha Nairobi
4:00 – 4:20	TAFSIRI NA UKALIMANI KATIKA DINI: Faida na changamoto katika uenezaji wa dini	Alfred Mtawali CAN, Translators
4:20-4:40	SAJILI NA MAWASILIANO KATIKA TAFSIRI YA MATINI ZA KISHERIA KWA KISWAHILI: MFANO WA KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE LA TAIFA	Vincent Magugu Chuo Kikuu cha Moi
4:40-5:00	Maswali, Maoni na Majinu	
5:00 – 5:15	Chai	
Sehemu ya Nane: Mawasilisho ya Makala Mwenyekiti: Dkt. Joseph Kariuki Katibu: Wilberforce, K		
5:15 – 5:35	TAFSIRI KATIKA ENZI YA UTANDAWAZI: MANUFAA NA CHANGAMOTO	Dkt. Toboso Mahero (Chuo Kikuu Kishirikishi cha Alupe) na Prof. Mosol Kandagor (Chuo Kikuu cha Moi)

5:35 – 5:55	AKIKI LINGANISHI WA UTEUZI WA MSAMIATI TIIKA USAWIRI WA WAHUSIKA MINTARAFU YA AGUZI MKUU WA SERIKALI (MWAKASAKA, 1979) MKAGUZI WA SERIKALI (MADUMULLA, 1999)	Dkt. Sophia Serem na Dkt. Jane Biama Chuo Kikuu cha Moi
5:55 – 6:15	TAFSIRI NA UHAKIKI WA DISKOSI	Prof. S. M. Obuchi Chuo Kikuu cha Moi
6:20 – 6:40	Nafasi za Tafsiri na Ukalimani katika karne ya 21	Dkt. Angela Sawe Chuo Kikuu cha Kabarak
6:40-7:00	Maswali, Maoni na Majibu	
7:00 – 8:00	Chamcha	
Sehemu ya Tisa: Makala Elekezi 4 Dkt. Mwanakombo Mohamed Katibu: Dkt. Maher Toboso		
8:00 – 8:40	Lughamama na Dhana ya ‘Lugha -A’: Changamoto za Utambuaji wa Lugha ya wanafunzi Chaguliwa wa Tafsiri na Ukalimani Afrika	Prof. Jayne Mutiga Chuo Kikuu cha Nairobi
Sehemu ya Kumi: Mawasilisho ya Makala Mwenyekiti: Dkt. A. Opijah Katibu: Dkt. Magdaline Wafula		
8:40 – 9:00	UFUNDISHAJI WA TAFSIRI KATIKA VYUO VIKUU NCHINI KENYA: MCHANGO NA CHANGAMOTO	Dkt. Sarah Ngesu Chuo Kikuu cha South Eastern Kenya
9:00 – 9:20	Changamoto za tafsiri kati ya Kiswahili na Kiarabu katika viwango vya kisemantiki	Dkt. Mbwarali Kame Chuo Kikuu cha Moi
9:20-9:40	Maoni, Maswali na Majibu	Wote
Sehemu ya Kumi na Moja: Kufunga Warsha		
9:40-10:00	Muhtasari, hitimisho na Mapendekezo	Prof. Mosol Kandagor Mratibu wa Warsha
10:00 – 10:20	Kufunga Warsha	Prof. Tom Mboya Mratibu wa Taaluma Moi-ACC

Prof Jayne Mutiga

Chuo Kikuu cha Nairobi

**Lughamama na Dhana ya 'Lugha -A': Changamoto za Utambuaji
wa Lugha ya Wanafunzi Chaguliwa wa Tafsiri na Ukalimani
Afrika**

Lughamama kama dhana kwenye kioo cha wingi-lugha huwa na maana mbalimbali za kiisimu ikifasiliwa katika mikabala mbalimbali. Hili ni kutokana na ukweli kwamba, wingi-lugha huwa ni kiungo cha maisha na unatumikizwa kwa njia mbalimbali kwa utegemezi wa muktadha unapotokea.

Fasili ya lughamama katika Kaskakazini ya Kimataifa, kwa mfano, huenda kabisa isikubaliane na fasili yake katika Mashariki ya Kimataifa, haswa katika maeneo yenye wingi-lugha, ikiwemo Bara la Afrika.

Vinginevyo, dhana ya 'lugha-A' kama inavyofasiliwa katika Tafsiri na Ukalimani ni kwa msingi fulani na kwa mtazamo dhahiri na uwili-lugha wa mnenaji. Mtazamo huu una athari jinsi lugha na ujuzi wa lugha kama vile ukalimani na tafsiri unavyofunzwa. Mtazamo huu una athari jinsi lugha na ujuzi wa lugha kama vile somo la ukalimani pamoja na la tafsiri yanavyofunzwa katika bara la Afrika.

Wasilisho hili litaweka wazi jinsi ulewa mbalimbali wa dhana ya wingi-lugha unaweza kuchochea shughuli za ubainishaji wa 'lugha-'A' na lughamama ya mtu binafsi, haswa kwa kusudi la kutambua lugha kuu ya mtu huyo katika mtihani wa uteuzi wa wakalimani na watafsiri. Kwa kuzingatia wazo letu kuhusu hali ya lugha nchini Kenya, wasilisho hili, zaidi litaonyesha jinsi lugha inatumika kila siku nchini na kuonyesha jinsi hali hii inaleta changamoto katika uwekaji mipaka kati ya lughamama na lugha zingine za elimu na pia changamoto ambazo hili linaweza kuibua katika kubaini 'lugha -A' ya mtu binafsi.

Hadija Jilala

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Nafasi ya Tafsiri na Ukalimani katika Umajumui wa Kiafrika: Mafanikio, Changamoto, Suluhisho

Ufanisi wa mawasiliano ni msingi imara wa kufikia ukombozi wa kifikra, kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kumekuwepo na harakati za hitaji la kuwa na lugha ya umajumui wa Kiafrika ili kuweza kuwaunganisha Waafrika na hatimaye kufikia maendeleo endelevu. Katika harakati hizo, mjadala mkubwa ni kuwa na lugha ambayo itatumika katika mawasiliano na kuwa kiungo cha kuwaunganisha Waafrika. Lugha ya Kiswahili imetajwa na wanazuoni kadhaa kama vile Wole Soyinka, Ayi Kwei Armah, Mulokozi, Mutembei na wengine huku wakisisitiza kwamba Kiswahili ndiyo lugha yenye sifa na inayofaa kuwa lugha ya Ukombozi, Umoja, Umajumui na hatimaye Muungano wa Afrika yote. Hata hivyo, tunapozungumzia lugha ya umajumui wa Afrika hatuwezi kuepuka kuhusisha harakati hizi na tafsiri na ukalimani wa lugha na fasihi za Kiafrika. Hii ina maana kwamba, harakati za lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya umajumui wa Afrika haziwezi kutenganishwa na masuala ya tafsiri na ukalimani hasa katika asasi za kiserikali za umoja na ushirikiano wa nchi za Afrika kama vile EAC, OAU, AU na SADC. Hivyo basi, makala hii inahusu dhima na nafasi ya tafsiri na ukalimani katika kufikia umajumui wa Kiafrika kwa kuangazia mafanikio, changamoto na suluhisho. Hoja yetu ni kwamba nchi za Afrika ni nchi zenyenye lugha zake ambazo zimefungamana na utamaduni mahsusini wa jamii husika. Hivyo, tunahitaji kuwa na mikakati madhubuti itakayohusisha mbinu faafu na ufanisi wa tafsiri na ukalimani ndiyo itakayotuwezesha kufanikisha mawasiliano kuhusu masuala ya kiafrika na hatimaye kufikia maendeleo ya Waafrika. Hatuwezi kuwaunganisha waafrika bila kuwa na lugha moja inayowezesha mawasiliano na mawasiliano hayo hayawezi kuwa imara bila kuwa na mchakato madhubuti wa tafsiri na ukalimani ambao utarahisisha mawasiliano ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Hivyo, umoja na utambulisho wa Mwfrika kuitia lugha hauwezi kufikiwa bila kuwa na kiungo thabiti cha utamaduni na lugha. Hivyo mustakabali wa Kiswahili kama lugha ya umajumui wa Kiafrika imefungamanishwa na mustakabali wa michakato imara ya tafsiri na ukalimani.

Caroline Asiimwe

Chuo Kikuu cha Makerere

Ufasiri katika Sekta ya Sheria nchini Uganda: Changamoto na Mustakabali

Ufasiri mahakamani ni shughuli inayoambatana na matumizi ya lugha katika mazingira ya wingi lugha. Lugha ni nyenzo muhimu inayowezesha mawasiliano kuhusu jambo lolote la maendeleo katika jamii. Ukosefu wa mawasiliano husababisha ukosefu wa haki na baadhi ya matabaka na makundi ya kijamii jambo linalosababisha utofauti unaozua migogoro ambayo inaathiri maendeleo. Makala hii inatathmini shughuli ya mawasiliano mahakamani nchini Uganda kwa kuegemea lengo la 16 la malengo ya maendeleo endelevu. Kwa kuwa lengo hili linayapa kipaumbele masuala ya haki za binadamu, inabainika wazi kwamba raia wa Nchi Wanachama wa Jumuyia ya Afrika Mashariki wanahitaji huduma ya ufasiri kutoka lugha za kigeni kwenda Kiswahili ili kupata haki na kufaidi malengo ya maendeleo endelevu. Licha ya kwamba kuna haja ya kutekeleza lengo hili, bado kuna changamoto ya mawasiliano mahakamani ambayo kwa sasa yanaegemea ufasiri. Ufasiri ni nyenzo ambayo ingewawezesha watu katika mazingira ya wingi lugha kupata haki kisheria na kushiriki katika shughuli za maendeleo. Hata hivyo tunajiuliza; je, shughuli hii inatekelezwaje mahakamani? Inatekelezwa na nani? Ni nani anaiyeratibu? Mawasiliano na usahihi ni wa kiwango gani? Kuna sera yoyote inayohusu ukalimani mahakamani? Kwa kutumia nadharia ya ufasiri (interpretive theory), makala hii inahoji kwamba pamoja na kwamba kuna haja ya kuwa na sera ya ufasiri katika sekta ya afya, kuna haja ya mfasiri kuwa na ujuzi wa taaluma ya sheria na taratibu zake, umilisi na ufundu wa lugha unaofaa ili aweze kutoa huduma na kuwezesha upatikanaji wa haki.

Leonard Chacha Mwita

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Uwezekano ya Kiswahili kutumika kama Lugha ya Sheria Nchini Kenya

Katiba ya Kenya 2010 ilikifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi, sawa na Kiingereza. Katika juhudini za kutekeleza tamko hilo la kikatiba, katika mwaka 2012, shirika la *National Council for Law Reporting* (NCLR) lilitoa tangazo likiomba wataalamu watume mapendekezo ili kushiriki katika kutafsiri hati zote za kisheria nchini Kenya kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, na kuunda tovuti ya kitengo cha sheria yenye lugha mbili: Kiingereza na Kiswahili. Jambo hili halikuwahi kutimia. Hata hivyo, lilitoa mwanya wa kufikiria juu ya uwezekano wa kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika kitengo cha sheria nchini Kenya. Makala hii inakagua hali halisi ya lugha ya sheria nchini Kenya na utayari wa kukitumia Kiswahili katika mfumo wa sheria. Inagusia masuala ya tafsiri ya hati mbalimbali za kisheria na ukalimani katika mahakama nchini Kenya. Matumizi ya Kiswahili katika mfumo wa sheria hasa mahakamani yatabainishwa na nafasi ya bunge katika kutunga sheria (ambazo zingewekwa katika tovuti iliyotajwa hapo juu) itajadiliwa. Nadharia ya Skopos itaongoza mjadala huu. Hii ni nadharia ya tafsiri inayozingatia uamilifu wa matini (Vermeer, 1978). Kupitia kwa nadharia hii itawekwa wazi kwa nini Kiswahili kinastahili kutumiwa katika uandishi wa sheria nchini Kenya. Mwisho, faida na changamoto za kukitumia Kiswahili kama lugha ya sheria zitadadavuliwa.

Susan Chebet-Choge

Chuo Kikuu Kishirikishi cha Koitaleel Samoei Mosoriot, Kenya

Tafsiri, Utohozi na Uakronimu katika Ukuzaji wa Istilahi za Utafiti wa Kiswahili katika Kiwango cha Uzamilifu

Tafsiri, utohozi na uakronimu ni mbinu muhimu ambazo zimetumika kwa muda mrefu katika ukuzaji wa istilahi katika utafiti wa Kiswahili. Mbinu hizi zimetumika kwa sababu marejeleo na dhana nyingi za utafiti zimo katika Kiingereza ama lugha zingine za kigeni. Ili kukuza tafiti za Kiswahili, wanafunzi wamelazimika wanapoandaa miradi na tasnifu zao kuunda istilahi kwa kutafsiri na kutohoa isitlahi za utafiti kutoka Kiingereza ama lugha zingine kuja kwa Kiswahili na kwa kutumia pia mbimu ya uakronimu. Makala hii itachunguza jinsi mbinu hizi za uibuaji wa istilahi zilivyotumiwa kukuza istilahi katika tafiti za Kiswahili kwenye kiwango cha uzamilifu.

Gakuo Joseph Kariuki

Chuo Kikuu Kishirikishi cha Bomet

Changamoto za Tafsiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mfano wa “Nitaolewa Nikipenda” (Ngugi wa Thiong'o)

Makala haya yanajihusisha na tathmini za ufasiri fanikivu katika fasihi ya Kiswahili. Tafsiri fanikivu ni tafsiri inayotosheleza kanuni ya mguso sawa baina ya matini ya lugha asilia na ile pokezi. Tafsiri ni mchakato wa uhamishaji ujumbe kutoka lugha moja hadi nyingine na ambao hujizatiti kutobatilisha maana asili iliyokusudiwa na kama ilivyokusudiwa katika matini ya lugha chasili. Tunakusudia kutalii namna uhawilishaji maana na mchakato wake unavyopelekea ufasiri na uelewekaji wa matini ya fasihi kutoka lugha chasili ya Kiingereza hadi lugha pokezi ya Kiswahili. Ili kufanya hivyo, tutachunguza mitindo ya lugha na miktadha ya kitamaduni na mawasiliano hususan katika nakala ya Kiingereza na ile ya Kiswahili ya *Nitaolewa Nikipenda* yake Ngugi wa Thiong'o kuona ni vipi changamoto za tafsiri zinaweza kupelekeea wasomaji kuelewa au kufasiri maandishi vilivyo au visivyo kupata maana zilizokusudiwa na mwandishi. Tutaona ni vipi mtafsiri wa kazi hii amejizatiti kuboresha mawasiliano kwa matumizi ya visawe vya maana katika lugha mbili yaani Kiingereza na Kiswahili. Tutatathmini vilevile namna hadhira ya wapokezi wa matini ya Kiswahili inavyofasiri na kuelewa maana zinazowasilishwa. Ni matumaini yetu kwamba Makala haya yatakuwa kurunzi kwa wadau wa fasihi ya Kiswahili kupambana na changamoto za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili pamoja na kudhihirisha mchango wa tafsiri kwa lugha ya Kiswahili na fasihi yake kwa jumla.

Gitonga Josephat John

Chuo Kikuu cha Nairobi

Tafsiri kama Daraja la Utoshelevu wa Chakula Barani Afrika

Kwa muda mrefu, taaluma ya tafsiri imejikita kiatika masuala mbalilimbali ya mawasiliano na ubora wake, ila haijashughulikia kikamalifu kwa suala la iwapo ina msaada wowote katika kujikimu kwa Maisha ya binadamu haswa walio na lugha asilia kama Afrika. Tafsiri za Makala, miswada, vitabu, majarida, vipeperushi na hata mabango kuhusu mada tofauti tofauti zikiwemo, sheria, dini, mahusiano ya kimataifa, mahusianao ya kijamii na mengineo zimemnufaisha binadamu katika kuelewa ulimwengu wake. Basi, vivyo hivyo inatakikana tafsiri imkimu binadamu kimaisha katika utoshelevu wake wa chakula na mahitaji mengingine ya msingi. Ili kuhakikisha kuna utoshelevu wa chakula na kuimarisha kilimo katika bara la Afrika, ni sharti lugha asilia zitumikizwe kikamilifu. Binadamu hung'amua vyema zaidi anapoelezwa kwa lugha anayoimudu kabisa. Maelezo kuhusu kilimo bora na mbinu za kisasa za ukulima zinanahitaji kumfikia mkulima kwa uelewa wa moja kwa moja bila yeye kutafuta maana kwingineko. Hivyo basi tafsiri ya matumizi ya pambejeo za kilimo, maradhi mbalimbali ya mifugo na mimea, aina mbalimbali za mime, dawa za kunyunyizia mimea na za kutibu maradhi ya mifugo na haswa mchakato mzima wa kilimo itakuwa ya manufaa kwa safari ya kujitosheleza kwa chakula barani Afrika. Kwa kuongozwa na nadharia ya Skopos inayoangazia tafsiri kama kusudi na inayoongozwa na dhana ya utekelezi katika mihimili ya kusudi, wiano wa matini lengwa ukitokana na wiano wa matini chanzi pamoja na utendakazi wa matini lengwa, suala nzima la tafsiri na utoshelevu wa chakula linajitokeza. Nadharia hii ina msaada wa kuchanganua ni kwa nini tafsiri iliyolengwa inahitajika katika sekta nzima ya kilimo na hatma yake ya kuwawezesha wakulima ambao hawawezi kungamua istilahi za kitaaluma zinazokuwa kizingiti kwa katika suala nzima la uzalishaji wa chakula na uongezaji thamani kwa bidhaa za vyakula na mifugo. Kuweka bayana maana katika lugha asili za Afrika ni jukumu endelevu litakalokuwa na matokeo chanya kwa kuyawezesha mataifa ya Afrika kukabiliana na tatizo la mara kwa mara la ukosefu wa chakula bora, kinachotosha na kinachomudika. Tafsiri inapaswa kuchangia kwa malengo endelevu ya maendeleo katika taaluma ya kilimo na uzalishaji wa bidhaa za mimea na mifugo. Tafsiri tendaji inahitaji kutiliwa maanani ili iwe mojawapo wa suluhi ya matatizo yanayomkumba binadamu.

Mbwrali K. Mboramad

Chuo Kikuu cha Moi

Tatizo la Tafsiri kati ya Kiswahili na Kiarabu katika Viwango vya Kisemantiki

Tatizo la tafsiri baina ya Kiarabu na Kiswahili linakuja katika viwango tofauti tofauti, licha ya kufanana baina ya lugha hizi mbili katika baadhi ya hali, kuna tofauti katika kiwango cha kimofolojia, kiwango cha kisemantiki na kiwango cha kitamaduni, na matatizo makubwa yanawakumba wale wanaotekeleza mchakato wa kutafsiri au wale wanaojifunza Kiarabu wakiwa wa lugha hiyo. Kuna pia ugumu mwengine wa matumizi ya kamusi katika lugha zote mbili, mkalimani wa Kiswahili akiwa na dhana potofu ya ilinganishi kimaana katika lugha ya Kiarabu, hivyo kulitafsiri jinsi lilivyo katika lugha ya Kiarabu na maana linganishi katika Kiswahili kupotea, makala itaangazia matatizo yanayo mkumba mkalimani wa Kiswahili katika kuyatafsiri manebo ya Kiswahili yalio na ukuruba wa kimaana na Kiarabu ugumu unao jitokeza katika kuwasilisha ujumbe wa lugha hizi mbili katika ukalimani.

Alfred Mtawali

CAN-Translators

Tafsiri na Ukalimani katika Dini: Faida na Changamoto katika Uenezaji wa Dini

Tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo zina mchango mkubwa katika uenezaji wa dini mbalimbali Afrika na duniani kwa jumla. Hakuna dini ambayo imejipatia wafuasi pasipo kuhusisha watafsiri na wakalimani. Sikukuu ya Kimataifa ya Tafsiri kwa Kiingereza International Translation Day ambayo husheherekwa kila tarehe 30 mwezi Septemba ilianzishwa na mtafsiri mtajika wa Biblia St Jerome. Wasilisho hili litaangazia historia ya utafsiri katika dini, mateso waliyopitia watafsiri, matokeo ya kazi yao, hatua zilizopigwa kufkia sasa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya kiteknolojia, changamoto na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukuza taalum hii na vile vile kuwalinda watafsiri. Katika taaluma ya ukalimani, wasilisho litaangazia aina mbali mbali za ukalimani, na hatimaye kuchambua kwa undani mtindo wa ukalimani unaotumika zaidi katika dini, faida zake pamoja na changamoto zilizoko katika ukalimani wa aina hii. Aidha vifaa vinavyotumika katika ukalimani vitaangaziwa. Wasilisho hili pia litataja na kuzungumzia nadharia kadhaa zinazohusu tafsiri katika dini, sifa za tafsiri nzuri na aina za tafsiri zilizoko sasa hivi na mtindo wa tafsiri hizo. Hatimaye, suala linguine litakalomulikwa ni tafsiri katika dini kama kitega uchumi, njia ya kukuza hadhi ya jamii lengwa zinazopokea tafsiri, kuhifadhi lugha, uandaaji wa kamusi, utafiti wa lugha, uandikaji wa alfabeti na maendeleo ya jamii.

Mwanakombo Mohamed

Chuo Kikuu cha Moi

Tafsiri na Nafasi yake katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili

Makala hii inatathmini dhima ya tafsiri katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Nafasi hii ni ya kihistoria kwa sababu imeoana na chimbuko la fasihi katika tanzu zake zote. Mwansoko (2006), anaifasili 'tafsiri kuwa ni zoezi la uhawilishaji wa mawazo katika maandishi kutoka lugha moja hadi nyingine.' Tukiongozwa na nadharia ya Antonio Candido kuhusu dhima ya tafsiri katika fasihi na jamii (1988), utafiti huu unachunguza historia ya tafsiri katika fasihi ya Kiswahili tangu karne ya 19 hadi leo. Tafsiri zimejitokeza kama kipengele cha kimsingi katika chimbuko na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu umegawika katika sehemu nne: Kwanza, tumechunguza nadharia ya mfumo wa fasihi kama ilivyoasisiwa na Antonio Candido. Pili, tumeangazia historia ya tafsiri za kwanza kwa Kiswahili. Tatu, tumetathmini vipindi vya kihistoria vya tafsiri katika Afrika Mashariki kuanzia karne 19. Mwisho, tumeziezea kazi adhimu za tafsiri katika fasihi ya Kiswahili. Makala imehitimishwa kwa kutoa mchango wa tafsiri katika fasihi ya Kiswahili.

Miriam Mwita

Chuo Kikuu cha Mashariki mwa Afrika, Baraton

Dhima ya Tafsiri na Ukalimani katika Maendeleo: Mtazamo wa Kidayakronia

Taaluma ya tafsiri na ukalimani imewahi kushughulikiwa na wataalamu wengi watajika. Katika kushughulika kwao, wameafikiana kuwa tafsiri ni shughuli changamano na kwa sababu hiyo, tafsiri ni mchakato wa kuhamisha ujumbe katika maandishi, pamoja na uamilifu wake kutoka kwa lughachasili hadi kwa lugha lengwa kulingana na isimu, muktadha na utamaduni wa lugha zote mbili. Vilevile, ukalimani ni uhamishaji wa ujumbe unaopatikana katika mazungumzo au maongezi, pamoja na uamilifu wake kutoka lugha chasili hadi lugha lengwa huku isimu, utamaduni na muktadha wa jamii husika ikizingatiwa. Ukweli huu unapotukabili, tunaelewa kuwa, umuhimu na dhima ya tafsiri na ukalimani umekita katika matumizi ya lugha za watu wasiokuwa wa jamii moja kwa lengo sio tu la kuwaunganisha bali pia kuwashirikisha katika shughuli na hali anuwai. Kupitia kwa tafsiri na ukalimani, watu wa mataifa mabalimbali huweza kuelewana na kushirikiana katika shughuli kama vile biashara, ndoa mseto, elimu, michezo na hata kutazama na kusikiliza habari kutoka mataifa mengine. Katika muktadha huu, tafsiri na ukalimani huwa na dhima kubwa sana katika nyanja ya maendeleo. Katika wasilisho hili, azma yetu ni kuonyesha kuwa tangu zamani, tafsiri na ukalimani ni taaluma ambazo zimetegemewa duniani kuendeleza mataifa mabalimbali katika nyanja tofauti. Aidha, ili kuona dhima na uamilifu wa tafsiri na ukalimani katika maendeleo, tunanuia kutumia mtazamo wa kidayakronia. Mtazamo huu, utatuwezesha kudadisi mambo mseto yanayoitinga taaluma ya tafsiri na ukalimani. Aidha, changamoto zilizopo na mapendekezo ya tatuzi zake.

Maneno Makuu: *Tafsri, Ukalimani, Maendeleo, Isimu, Dayakronia*

Sarah Ngusu

Chuo Kikuu cha South Eastern-Kenya

Ufundishaji wa Tafsiri katika Vyuo Vikuu nchini Kenya: Mchango na Changamoto

Kuna lugha nyingi duniani ambazo hukwamisha mawasiliano baina ya watu. Suluhu ya hali hii hupatikana katika tafsiri na ukalimani. Tafsiri na ukalimani ni taaluma zinazowasaidia wanadamu kuelewana, kuelewa tamaduni za wengine na kuelewa maendeleo ya wengine. Katika hali hii, tafsiri na ukalimani zimeufanya ulimwengu kuwa “kijiji” kimoja na zimeechochea jitihada mbalimbali za kuandaa wataalamu wa nyuga hizo. Maandalizi haya yamekuwa yakifanyika katika vyuo vikuu vya Kenya ambavyo hufundisha kozi za tafsiri katika viwango mbalimbali. Ikihusika na tafsiri, makala hii inadadidsi ufundishaji wa tafsiri na jinsi ya kutathmini umilisi na umahiri wa wanafunzi wanaosoma somo la tafsiri. Utafiti wa awali umeonesha kwamba kozi za tafsiri hufanywa katika vyuo vikuu mbalimbali nchini Kenya katika viwango vya digrii ya awali, uzamili na uzamivu. Hata hivyo, mapitio ya maandiko yanaonesha kwamba kuna tafiti chache kuhusu ufundishaji na tathnini ya tafsiri kama taaluma inayojitegemea nchini Kenya. Ufundishaji wa tafsiri ni changamani na wa kipekee. Mwalimu wa tafsiri ana kazi mara difu, kufundisha tafsiri kinadharia na kufundisha tafsiri kiutendaji. Data za makala hii zilikusanywa kupitia mbinu za hojaji na usaili wa kiteknolojia. Watoataarifa 50 ambaao walikuwa wahadhiri wa kozi za tafsiri katika vyuo mbalimbali nchini Kenya walishiriki katika utafiti huu. Matokeo yanaonesha kwamba vyuo vikuu mbalimbali nchini Kenya havifundishi tafsiri kama taaluma bali kama kozi chache tu katika viwango mbalimbali. Aidha, kozi za tafsiri zinazofundishwa ni chache kuweza kumpa mwanafunzi umahiri katika tafsiri. Vilevile, mitaala ya tafsiri imekitwa katika kufundisha masuala ya kinadharia zaidi na haimpi mwanafunzi fursa ya kufanya utendaji. Pia, baadhi ya walimu wanaofundisha tafsiri hawajasomea tafsiri kwa kina. Aidha, kuna changamoto za kinadharia katika mchakato wa kutathmini kazi za wanafunzi za tafsiri kwani hakuna kigezo maalum cha kutumika katika tathmini za tafsiri. Inapendekezwa kwamba ni muhimu kuandaa mtaala wa kufundisha tafsiri kama taaluma na kuwa na warsha za mara kwa mara za wahadhiri wanaofundisha tafsiri ili kuelekezana katika ufundishaji.

Maneno Makuu: *Ufundishaji, Tafsiri, Tathmini, Vyuo Vikuu*

Samuel M. Obuchi

Chuo Kikuu cha cha Moi

Tafsiri na Uhakiki wa Diskosi

Kuna uhusiano mkubwa sana kati ya Diskosi na Tafsiri. Katika makala haya, ninafahamisha kuwa Diskosi ni ama matini iliyandoikwa au inayosemwa, popote na yejote. Katika kuihakiki Diskosi yoyote iliyandoikwa au inayosemwa na pengine kunakiliwa, mhakiki anafaa kuihakiki kwa kuzingatia masuala mbalimbali yanayohusu uhakiki wa sampuli hii, kwa mfano: Matini ilisemwa au iliandikwa na nani? Je, mada ya matini husika inaegemea mrengo au itikadi gani? Je, nani alikusudiwa kuipata au kuipokea matini hiyo, na kwa nini? Mwandishi wa matini hiyo alidhamiria kuafikia malengo gani hasa? Je, yasiyoeleweka au yasiyo wazi katika matini inayohakikiwa yanaweza kunyooshwa vipi kwa kurejelea matini au diskosi asilia? Katika kuyajibu maswali haya na mengine, ni muhimu anayehakiki matini husika awe tayari kuirejelea matini asilia, hasa inapotokea kuwa pengine mtafsiri alikumbwa na mapendeleo au changamoto fulani katika kutafsiri alivyotafsiri. Katika makala haya basi, tutaangazia baadhi ya matatizo ambayo huwakumba wahakiki wa diskosi mbalimbali zilizotafsiriwa na namna ya kukabiliana nazo kwa lengo la kuhakikisha kuwa uhakiki wake unakubalika na kuchukuana vizuri na matamanio ya mwandishi wake asilia huku akiwa mwaminifu kwa hadhira yake.

Kenneth Simala

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Tafsiri ya Kiswahili katika Mwongo wa Lugha Asili (2022 - 2032)

Makala hii inajadili mchango wa tafsiri kwa maendeleo na ukuaji wa taaluma ya Kiswahili katika miaka kumi ijaayo. Mwongo wa 2022 -2032 umetengwa na kutangazwa na Umoja wa Mataifa (UN) kuititia Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi, Utamaduni na Mawasiliano (UNESCO) kuwa kipindi mahsusini cha kuangazia lugha asili na kutafakari namna ya kuziimarisha na kuziendezea. Hoja kuu katika makala hii ni kwamba kwa miaka kumi ijaayo, Kiswahili kina fursa kubwa ya kujiendezea na kuendeleza lugha nyingine kuititia manufaa ya tafsiri. Makala inapendekeza haja ya kuweka sera zifaazo na mipango muafaka ya kukijenga Kiswahili kimataifa kwa misingi ya tafsiri.

Sophia Jeptoo Serem na Jane Biama

Chuo Kikuu cha Eldoret

Uhakiki Linganishi wa Uteuzi wa Msamiati katika Usawiri wa Wahusika: Mintarafu ya “Mkaguzi Mkuu wa Serikali” (mwakasaka, 1979) na “Mkaguzi wa Serikali” (Madumulla, 1999)

Makala haya yanalenga kutambua tofauti za matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa ujumbe na uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (MMS) (Mwakasaka, 1979) na *Mkaguzi wa Serikali*, (MS) (Madumulla, 1999). Aidha makala yanahakiki kiulinganishi mbinu za lugha katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*, kuchambua kiulinganishi matumizi ya lugha katika uwasilishaji wa ujumbe katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*, kuhakiki kiulinganishi uteuzi wa msamiati katika usawiri wa wahusika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mkaguzi wa Serikali*. Nadharia ya Uamilifu katika tafsiri mtazamo wa kuhakiki matini uliopendekezwa na Reiss ndiyo itakayoongoza utafiti huu. Mihimili mikuu ya mtazamo huu ni mitatu nayo ni: utambuzi wa kuhakikisha kuwa kuna utoshelevu wa kisemantiki, kisarufi na kimtindo katika lugha lengwa kwa minajili ya kuuwasilisha uujumbe kwa wapokeaji wake, Kaida za matumizi ya lugha na uelewa ya kwamba kwa ajili ya mawasiliano maana ya neno hurejelewa kwa kuhusishwa na maneno mengine yanayohusiana na mada au muktadha wa diskosi unaozungumziwa, kwamba matini pokezi inatarajiwa kudhihirisha mguso sawa na ule unaojitokeza katika matini asilia.

Toboso Mahero na Mosol Kandagor

*Chuo Kikuu cha Alupe
Chuo Kikuu cha Moi*

Tafsiri katika Enzi ya Utandawazi: Manufaa na Changamoto

Utandawazi ulioanza kama mchakato wa kiuchumi sasa umetawala takribani kila sehemu ya maisha ya mwanadamu katika viwango vya kitaifa na kimataifa. Utandawazi umefuta mipaka ya kimataifa na kuyalazimu mataifa mbalimbali kutoa vikwazo vya maingiliano na watu wa mataifa mengine. Kutokana na hatua hii, ulimwengu sasa umekuwa kiambو kimoja chenye watu wasioweza kutenganika. Sasa, hakuna maarifa ya taifa moja wala jamii moja kwa kuwa maarifa yote muhimu hata yale yaliyovumbuliwa na mtu binafsi sasa yanasantaa kwa haraka na kuwa ya kilimwengu. Kutegemeana kwa watu wa ulimwengu kumesababisha mitagusano mingi katika misingi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Maingiliano huria kati ya watu takribani bilioni 7.9 wa ulimwengu na wanaozungumza takribani lugha 6,000, yamezua mahitaji makubwa ya tafsiri ulimwenguni kote. Makala haya ni mjadala kuhusu nafasi ya tafsiri katika ulimwengu unaotamalakiwa na utandawazi. Makala yanatalii manufaa yanayoletwa na tafsiri na kuangaza changamoto zinazokabili taaluma nzima ikiwemo michakato ya tafsiri. Hitimisho la makala ni kwamba changamoto zilizopo, zinazoathiri taaluma, hazipaswi kuwa chanzo cha maangamizi ya yake.

Maneno muhimu: *Tafsiri, Ukalimani, Utandawazi, Taaluma*

Magugu V. Njeru

Chuo Kikuu cha Moi

Sajili na Mawasiliano katika Tafsiri ya Matini za Kisheria kwa Kiswahili: Mfano wa Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa

Jambo la msingi ambalo hubainika katika taaluma ya tafsiri aghalabu huwa ni haja ya kuzingatia maana iliyomo katika matini chanzi pamoja na kuwezesha matini tafsiri kuwasiliana na kudumisha uamilifu uliokusudiwa. Katika kutafsiri matini za kisheria, kama ilivyo Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa la Kenya, suala la sajili ni la kimsingi hasa kutokana na sifa za lugha ya kisheria inayotumia; sintaksia changamano yenye uradidi wa kufafanua dhana, matumizi ya maneno ya kale na hata ya kigeni, pamoja na upekee wa maana zinazofumbatwa na maneno yanayotumiwa. Kinyume na lugha katika miktadha kama vile mawasiliano ya jumla au hata matangazo ya biashara ambapo muhtasari na uchukulio ni dhana zinazotumiwa ili kubana idadi ya maneno yanayotumiwa, katika sajili ya sheria, kuna uradidi wa kileksia na maelezo ya kina kwa lengo la kuepuka utata wa kimaana. Upekee huu wa lugha ya kisheria unaibua changamoto anuwai kwa mtafsiri. Licha ya kutumia mwelekeo wa tafsiri sisisi ambao unalenga kudumisha uaminifu kwa matini chanzi, suala la isimu katika sajili ya kisheria yaani; sintaksia, mofolojia na semantiki, huibua changamoto za kipekee katika kuwasilisha maana kwa njia inayodumisha uaminifu na kuwezesha mawasiliano. makala hii Imetalii suala la tafsiri ya matini za kisheria kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kwa kujikita kwa tafsiri ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa la Kenya. Imeangazia jinsi vipengele vya sajili vinavyoathiri mawasiliano pamoja na kueleza baadhi ya mikakati iliyotumiwa katika kuhakikisha kuwa maana ya matini chanzi imedumishwa kadri ilivyowezekana katika tafsiri ya Kiswahili. Makala hii inalenga kuweka msingi kwa uhakiki wa tafsiri iliyoteklezwa kwa Kanuni za Kudumu za Bunge la Taifa hasa kwa kutoa taarifa za kiusuli za mchakato mzima wa tafsiri. Aidha, imeeleza baadhi ya maamuzi ya kileksia yaliyofanywa pamoja na miundo ya kisintaksia iliyotumiwa. Haya ni kutokana na tajriba za mwandishi kama mmoja wa wanajopo walioshughulikia tafsiri hii.

MOI UNIVERSITY AFRICAN CLUSTER CENTRE

